

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



“Mtaa wa Bagara
S.L.P. 386,
27103 MANYARA,
Barua Pepe: rbcmanyara@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

MANYARA – SEPT 25, 2020

**MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI WILAYA BABATI
KUFIKISHWA MAHAKAMANI KWA RUSHWA**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoa wa Manyara inamshikilia Mahelele Mussa ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Babati kwa makosa ya kudai na kupokea rushwa ya shilingi laki tano (Sh.500,000/=) kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya Mwaka 2007.

Awali tulipokea taarifa kutoka kwa mlalamikaji (jina linahifadhiwa) ambaye alishinda kesi yake katika moja ya mabaraza ya kata Mkoani Manyara na shauri hilo kukatiwa rufaa katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Babati

Ilidaiwa kuwa, Kesi hiyo ya rufaa imekuwepo mahakamani hapo tangu mwaka 2016 bila kutolewa uamuzi na mlalamikaji wetu alipokutana na Mwenyekiti huyo wa Baraza kuulizia kuhusu sababu za kuchelewa huko kwa uamuzi katika shauri hilo ambalo yeye ni mshindi kwenye Baraza la Kata, alitakiwa kupeleka kiasi cha shilingi laki tano (Sh.500,000/=) ili aweze kumfanyia upendeleo katika uamuzi wa rufaa hiyo.

Kutokana na imani waliyo nayo wananchi walio wengi wa Mkoa wa Manyara kwa TAKUKURU, mwananchi huyo alitoa taarifa hizo kwetu zilizopelekea kukamatwa kwa mwenyekiti huyo kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa hiyo. Mwenyekiti huyo tunamshikilia na anatarajiwa kufikishwa Mahakamani tarehe 29/09/2020 baada ya kukamilisha mambo machache ya kiuchunguzi yaliyo salia.

Wakati huohuo ofisi yetu ya wilaya ya Hanang jana tarehe 24/9/2020 katika kufuatilia ujenzi wa kituo cha afya cha Hirbadaw ilibaini kuwa mkandarasi aliyepewa kazi ya kuweka milango 83 kwenye kituo hicho kwa gharama ya shilingi milioni

*All letters be addressed to Regional Bureau Chief Bagara Miomboni Street, P.O. Box 386, 27103 MANYARA You may also communicate with us through Hotline: 113, **instagram:** takukuru.tz, **Facebook:** TakukuruTZ, **Twitter:** TAKUKURU.TZ,*

Online TV: TAKUKURUTV

ishirini na nane [28,000,000/=] aliweka milango ambayo ipo chini ya kiwango kwa mjibu wa mkataba ambao aliingia na Halmashauri ya wilaya ya Hanang.

Ufuatiliaji uliofanywa na maafisa wetu wa wilaya ya Hanang ulibaini kuwa mkandarasi huyo, Ndugu Ayubu Lyaka aliingia mkataba na Halmashauri ya wilaya ya Hanang tangu mwaka jana 2019 ili aweke milango 83 katika kituo hicho cha afya kwa gharama ya shilingi 28,000,000/= na alitakiwa aweke milango ya mbao ngumu na yenye ubora, badalayake aliweka milango ya mbao laini na mbichi na kuipaka rangi; kutokana na hali hiyo wakati wa ukaguzi milango mingi ilikuwa imeshapasuka na kupinda. Wakati huo mkandarasi alikuwa ameshalipwa jumla ya shilingi 14,000,000/= kati ya shilingi 28,000,000/= za mkataba.

Kwenye ufuatiliaji huo na kutokana na kasoro ambazo TAKUKURU ilibaini; ilimshirikisha Mhandisi anayesimamia mradi huo pamoja na Mkandarasi aliyeweka milango hiyo na kwa pamoja waliziona kasoro hizo. Kutokana na uwepo wa kasoro hizo **Mhandisi wa wilaya** anayesimamia ujenzi huo alimuamuru mzabuni aondoe milango yote 83 na aweke milango yenye ubora unaotakiwa kwa mjibu wa mkataba aliosani na Halmashauri.

Ni wito wetu kwa wazabuni wanaopewa zabuni wafanye kazi za serikali kwa kuzingatia mikataba na kwa ubora unaotakiwa, watumishi wa umma wenye wajibu wa kusimamia miradi ya serikali wasimamie miradi hiyo kwa ukaribu, umakini na uadilifu ili kuhakikisha miradi husika inathamani na inaaksi thamani ya fedha iliyotumika.

Ni Rai yetu kwa wananchi wa mkoa wa Manyara kuwa waendeleo kutoa taarifa kwa ofisi za TAKUKURU Wilaya na Mikoa zilizoko karibu nao au kwa namba yetu ya dharura 113 ambayo mwananchi hapaswi kulipa, taarifa hizo zitaiwezesha Serikali ya wanyonge inayoongozwa na Rais John Pombe Joseph Magufuri iendeleo kuwaondoa watumishi wachache waliosalia ambao bado wanaendeleza rushwa, dhuluma, ufisadi na ubadhilifu wa mali za umma

Imetolewa na:

ISDORY KYANDO
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M)
MANYARA

All letters be addressed to Regional Bureau Chief Bagara Miomboni Street, P.O. Box 386, 27103 MANYARA You may also communicate with us through Hotline: 113, **instagram:** takukuru.tz, **Facebook:** TakukuruTZ, **Twitter:** TAKUKURU.TZ,

Online TV: TAKUKURUTV